

SIRI YA MUNGU ILIYOFICHWA SASA IMEUNULIWA

Wakolosai 1: 15 – 19 “ Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika Yeye(mstari 17)

Sikiliza kile nabii wa mungu alivyosema juu ya hilo.

Sasa siri ya Mungu iliyofichwa aliyokuwa nayo kabla ya dunia kuanza Sasa, nyuma kule nyuma katika nia yake, kulikuwa na kitu fulani ambacho alikuwa anajaribu na alichokuwa akienda kukifanya, na alikuwa na lengo katika kulifanya hilo, ili aweze kujieleleza au kujitambulisha Yeye mwenyewe. Kwasababu kwanza hakukuwa hata na mwezi, nyota, chembechembe ndogo, molekuli au chochote. Yeye alikuwa Mungu. Lakini hakuwa Mungu hasa wakati huo, kwasababu Mungu ni kitu cha kuabudiwa na hapakuwa na kitu cha kumwabudu Yeye. Sasa katika nia Yake kuu alitaka hizi sifa zake zidhihirishwe. Na ndani yake kulikuwa na upendo, ndani yake kulikuwa na sifa ya Baba, ndani Yake kulikuwa na sifa ya kuwa Mwana, ndani Yake kulikuwa na sifa ya kuwa Mwokozi, ndani Yake kulikuwa na sifa ya Mponyaji. Na sifa hizi zote kuu ambazo tunazona zilidhihirishwa, zilikuwa ndani ya Mungu.

Kwa hiyo Mungu kwa mawazo yangu , kitu cha kwanza alichoumba ilikuwa ni malaika(Isaya 1 4:12 – 14) na hapo wakaanza kumwabudu Yeye na hilo lilimfanya Yeye kuwa Mungu. Naye akaanzia hapo. Na sasa, malaika walipo anza kumwabudu Yeye , hapo ilikuwa kabla hakujawa na hata chembechembe yeyote katika Ulimwengu, hakukuwa na chochote. Ilikuwa yote ni giza. Hakukuwa na jua au hakuna mwezi, hakuna nyota wala chochote; hapo alikuwa Mungu. Kama alivyomuuliza Ayubu, “ilikuwa wapi hapo nilipoweka misingi ya dunia? Wakati nyota za asubuhi walipoimba pamoja hapo wana wa Mungu walipopiga kelele za furaha? ulikuwa wapi? “(job 38:1-7). Hapo ilikuwa nyuma kule kabla ya ulimwengu.

Sasa, Mungu alikuwa na kusudi na siri iliyofichika. Alikuwa nayo niani Mwake kabla ya dunia haijaaza na vile ambavyo ilijifunua (au huwekwa wazi) yenyewe mpaka hapa chini wakati na saa tunayoishi. Unaona? Sasa utaelewa vizuri hapa na huendelea, naamini juu ya lile lililofanyika.

Siri kuu ya Mungu ya namna.....Ni siri, Yeye aliiweka kuwa siri,. Hakuna aliyejua chochote juu ya hiyo, hata malaika hawakuielewa hiyo, unaona? Yeye hakuifunua hiyo? Hiyo ndiyo sababu chini ya siri yetu ya saba, wakati ule muhuri wa saba ulipofunuliwa, kulikuwa na kimya(Ufunuo 8:1). Yesu alipokuwa hapa duniani, walitaka kujua ni wakati gani Yeye atakuja. Yeye alisema,”hiyo siyo.....Hata Mwana mwenyewe hajui itaenda kutokea lini

(Mathayo 24:36 : matendo 1:7).Unaona , Mungu anayo hiyo yote kwa ajili Yake Mwenyewe. Ni siri na ngurumo saba zilitoa sauti zao, na hata Yohana alikatazwa kuandika hilo kule kuja kwa Bwana(ufunuo 10:1-7). Hilo ndilo jambo ambalo Yeye hajalifunua bado, jinsi Yeye

atakavyokuja, na ni lini Yeye atakuja. Ni jambo zuri kwamba Yeye hajalifanya hilo. Hapana. Yeye amelionyesha au kulifunua kwa kila ulinganisho katika Biblia.

Kwa hiyo, Biblia yote ni ufunuo wa siri ya Mungu ndani ya Kristo. Biblia yote inaeleza lengo/kusudi moja ambalo Mungu alikuwa nalo, kusudi moja ambalo alitaka afanikishe katika Biblia, na katika matendo yote ya waaminio katika Biblia yalikuwa ni mifano na vielelezo vya lile kusudi/lengo alilokuwa nalo. Na sasa katika siku hizi za mwisho amelifunua hilo na kulionyesha hilo (ufunuo10:7). Na kwa msaada wa Mungu, tutalionga hilo hapa hapa. Kile Bwana alichokuwa nacho katika nia Yake wakati wote na amelieleza hilo.

Biblia ni kitabu cha unabii, Ni kitabu cha historia, ni kitabu cha mapenzi/upendo. Ni kitabu cha nyimbo, ni cha uzima, na ndani pale unampata Kristo. Yeye alikuwa ndani ya manabii, alikuwa katika Zaburi, Alikuwa katika historia, na Yeye pia katika Biblia ni mambo yale yajayo. Kwa hiyo alikuwepo kabla na baadae. Hiyo inamfanya Yeye kuwa nini? Yule yule jana, leo na hata milele (Waebrania 13:8).

Na unaingiza kitu fulani pale ambacho hakimfanyi Yeye kuwa yule yule wa jana leo na hata milele, utaenda wapi hapo? Una picha mbaya pale. Kwa sababu Yeye alikuwa historia na alikuwa manabii, alikuwa ni Zaburi, Yeye ni kila kitu. Na kama huwezi kumfanya Yeye kila kitu na yule yule. Picha yako itaonekanaje? Unalionga hilo? Vema.

Yeye ni yule yule, alikuwa ni wale manabii, Alikuwa ndani yao, alikuwa katika Zaburi, alikuwa katika historia, na Yeye ni mambo yote yajayo, ni yule yule jana, leo na hata milele (waebrania 13:8). Kama hivyo ndivyo alivyo, na tunaliamini hilo, au mnasemaje? Sasa kama yuko hivyo, hapo sasa inabidi Yeye awe ndiyo kitu kikuu cha mazungumzo yetu, cha mawazo yetu, cha kuimba kwetu, cha kutembea kwetu, Anapaswa kuwa kitu kikuu cha maisha yetu. Kama Yeye ni kitu kikuu cha maisha yetu. Kama Yeye ni kitu kikuu cha Biblia, na Biblia iliyo ndani yetu, hapo sasa anapaswa Yeye awe ni kanuni yetu kuu ya kila kitu ambacho tunakifanya, tunakisema, au tunachofikiria, lazima iwe ni Kristo. Hivyo ni sawa? Vema sasa. kwa kuwa tunafikiri hili, kwa kuwa amefanywa kichwa cha vitu vyote kwetu sisi.....(wakolosai 1:16-18). Wakolosai wamesema hivyo hapa. Yeye ni kichwa cha vitu vyote kwetu sisi kwa maana Yeye amekuwepo kwa ajili yetu, amabapo sisi tunaitwa ni vitu vyote, unasema inakuwaje kuhusu wenye dhambi? “Amefanywa kuwa hakimumu wa wenye dhambi, kama hatalikubali hilo. Yeye amefanywa utukufu kwa mwaminio ambaye analikubali hilo. kwa hiyo kuna vituVitu vyote viliumbwa na Yeye na kwa ajili Yake (warumi 11:36).

Na inachukuwa usiku kuelezea utukufu wa siku, inachukua vyombo visivyo vya utukufu kuelezea upendo na kujali kwa vyombo vya heshima(warumi 9:14-23). Inamchukuwa mwanamke mwovu amabaye anavaa nguo za kizinifu na kuuza utu wake, ili kumwelezea mwanamke msafi ambaye ni mwanamwali halisi unaona? Inamchukua mwizi na jambazi ndani ya mtu ili kuelezea uhalisi wa mwaminio wa ukweli. Mkristo halisi inachukua mnafiki kumwonyesha yule mwaminio, kile alichu.

Kwahiyo vitu vyote viliumbwa na Yeye. Na kwa kuwa Yeye amefanyika kuwa yote hakika yote kwa ajili yetu (2 kor. 4:15); vitu vyote vimeumbwa kwa na Yeye, sasa kwakuwa hilo ni kweli, kitambulisho chetu lazima kiwe na Yeye. Lazima tutambulishwe sisi wenyewe na Yeye kwa sababu Yeye amejitambulisha mwenyewe na sisi ni lazima tutambuliswe na Yeye kwa namna gani? Kwa kuishi kwa ajili Yake (warumi 14:7-8), siyo tu kukiri/kuungama. Angalia Mungu katika siri hii kuu iliyofichwa na kusudi lililo katika mambo matatu, Mungu katika siri yake kuu iliyokuwa imefichwa na ambayo alikuwa nayo kabla ya kuanza kwa dunia, alikuwa na kusudi lililo katika hali tatu ndani Yake, na sasa tunachotaka kukiendea ni nini hilo kusudi lililo katika hali tatu? Unaona? Sasa ninaamini kwa msaada wa mungu ambaye yupo hapa, Yeye atatuonyesha hilo.

Tunataka tufahamu ni nini hilo kusudi lililo katika hali tatu, jambo la kwanza lilikuwa Mungu alitaka kujifunua Yeye mwenyewe kwa watu, Yeye asingeweza kufanya hivyo kama jehova Mungu mkuu ambaye yuko katika kila mahali wakati, na milele. Asingeweza Yeye ni mkuu sana kuweza kufunuliwa kwa watu kwa sababu lingekuwa jambo la kisiri sana. Ni kwa namna gani kile kiumbe ambacho kamwe hakina mwanzo, kwamba kama ungeenda uvuke mduara wa miaka mia moja bilioni na trilioni na matrilioni ya miaka ya usafiri wa nuru na uendeleo nje huko katika kiwango kisicho na mwisho, niingie milele na kiumbe hiki kikuu ambacho kilikuwa vyote hivyo na bado kinadumu.....

Lakini kile alichotaka kufanya alipenda ule ubaba, kwa maana alikuwa Baba. Na njia pekee ambayo angeweza kuelezea huo ni kuwa Mwana wa adam. Hiyo ndiyo sababu Yesu alidumu akisema “Mwana wa Adam” (mathayo 8:20, 18:11). Unaona wengi wao hawakuelewa anazungumzia kitu gani lakini sasa mnanielewa?. Alitaka kujieleleza Yeye mwenyewe hilo lilikuwa moja ya moja ya malengo Yake makuu katika kusudi lile la hali tatu ambalo lilikuwa la kujielezea Mwenyewe, kujitambulisha Mwenyewe na wana adamu, kwa kujifunua Mwenyewe ndani ya Kristo (wakolosai 2:9-10)

Jambo la pili: kuchukua nafasi ya kwanza katika mwili wake wa waaminio ambao ni Bibi harusi wake, kwamba aishi ndani ya watu wake (wakolosai 1:18). Sasa angeweza kufanya hilo ndani ya Adamu na Hawa lakini dhambi iliwatenganisha wao, kwa hiyo sasa inabidi iwepo njia ya kuirudisha tena kule nyuma. Oh jamani, oh hili ni la kitajiri sana kwangu, ile tuu kuijaribu kulifikiria hilo! unaona? Unaona kile ambacho kilikuwa ni kusudi la Mungu?. Sasa, kwa nini asingewaacha Adamu na Hawa kama hivyo. Hapo sasa asingeweza kamwe kujieleza kile alichokuwa katika ukamilifu wa utimilifu wake, ukamilifu wa utimilifu wa sifa zake, kwa sababu.....Hapo Yeye angeweza kuwa Baba, hiyo ni kweli, lakini pia Yeye alikuwa ni Mkombozi. Unasema, unajuaje Yeye alikuwa hivyo? Yeye yuko hivyo kwa sababu nimepata ule uzoefu nae unaona, unauona?. Yeye ni Mwokozi, na inabidi alieleze hilo, naye angeweza kufanya hivyo?. Ni kwa kupitia tuu Kristo. Angewezaje Yeye kuwa Mwana? Ni kupita tuu Kristo angewezaje Yeye kuwa Mponyaji? Ni kupitia tuu Kristo unaona, vitu vyote vinajumlishwa ndani ya huyu mtu mmoja Yesu Kristo. Oh jamani.

Na ninapojaribu kufikiri hilo, ninaona tuu madhehebu yakipita mbali yasionekane mahali, kila kitu kinaondoka unaona?. Ninapooni kusudi kuu la Mungu; alijifunua Yeye Mwenyewe na alikuwa.....moja, kujifunua Mwenyewe katika Kristo, utimilifu wa Mungu

kwa jinsi ya mwili ndani ya watu ambao Yeye anaweza kuchukua nafasi ya kwanza, aliye mkuu na anayeongoza.

Kwanza, kujieleleza Mwenyewe kikamilifu; Mungu ndani ya Kristo. Pili, kuwa na nafasi ya kwanza kwa hili katika kanisa lake (ambalo ni mwili wake, yule bibi harusi)ku.....Aweze kuchukua nafasi ya kwanza kujieleleza Mwenyewe kupitia wao. Na la tatu, kuurudisha ufalme katika hali yake sahihi ambao ulianguka kwa sababu ya dhambi ya Adamu wa kwanza, kurudi tena kule nyuma alipotembea katika utulivu wa wakati wa jioni pamoja na watu wake, akizungumza nao, alikuwa na ushirika nao (mwanzo 3:8). Na sasa dhambi na kifo vimewatenganisha wao kutoka kwenye uwepo wake na utaratibu wake wa kujidhihirisha kabla ya kuwekwa misingi ya dunia kule kuelezea sifa zake alichokuwa.....Mungu, alidhihirishwa ndani ya Yesu Kristo, ambaye alikuwa ni vyote, Baba,Mwana na Roho Mtakatifu, ule ukamilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Sasa, ule itimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani ya kanisa, kule kuchukua nafasi ya kwanza vile vyote alivyokuwa Mungu alivimwaga katika Kristo. Na vile vyote alivyokuwa Kristo alivimwaga ndani ya kanisa, yule mwaminio, siyo dhehebu.

Sasa angalia tena. Sasa, lile kusudi lililo katika hali tatu ni nini? Kujidhihirisha Yeye Mwenyewe ndani ya Yesu Kristo, kuja katika mwili Yesu Kristo kuwa na nafasi ya kwanza katika nini? Kurudisha tena ile edeni, kuleta kile ambacho kimepotea. Ambacho ndicho kitu pekee kilichokuwa nje ya utaratibu, vitu vyake vyote vingine vilikuwa katika utaratibu. Na sasa, yule Kristo katika kanisa anafanywa ajulikane jambo lote ni ule ufunuo wa Mungu kumchukua Hawa tena nyuma kule katika hali yake sahihi tena na mumewe, na Mungu ni mume wa kanisa, na kanisa lake ni bibi harusi wake.

Angalia, Kristo ndani yako inamfanya Yeye kuwa kiini cha ufunuo. Kristo katika Biblia, inaifanya Biblia kuwa ufunuo mkamilifu wa kitu chote. Unaona kile Mungu anachojaribu kufanya?. Ni nini kule kuzaliwa mara ya pili basi? Unasema," Vema, ndugu Branham, ni nini kule kuzaliwa kwa pili? Ni kule kufunuliwa kwa Yesu Kristo kibinafsi kwako. Amen. Unaona? Siyo ulijiunga na kanisa, ulipeana mkono; umefanya kitu fulani tofauti, ulisema kanuni, uliahidi kuishi kwa utaratibu wa sheria; lakini Kristo, Bibilia.....Yeye ni Neno ambaye amefunuliwa kwako. Na haijalishi chochote kile ambacho mtu fulani atasema, kile kinachotendeka, ni Kristo. Mchungaji, kuhani, chochote kiwacho..... ni Kristo ndani yako (wakolosai 1;26-29). Huo ni ufunuo ambao kanisa lilijengwa juu yake. [1]

Sasa, Yeye anafunua mambo haya kwa ufahamu wake wa kimbele kwa wale aliowakusudia kwa mambo hayo; vinginevyo hawawezi kuliona hilo na bado hawawezi kuliona hilo (mathayo 13:10-12,waefeso 1:4-10). Ni wangapi walio wahi kuiona ile picha ya ngombe akiwa kichakani, ambayo inabidi uiangalie na kuiangalia? Uliwahi kuiona hiyo/ uliiona picha ya Kristo akiwa kichakani au katika anga au mawingu? Unaona yule mchoraji ameiweka kwa namna ambayo mpaka ukiiangalia kwa namna fulani. Vema sasa ukiiiona mara moja, huwezi kuangalia kitu kingine ila hiyo. Kila mara ukiiangalia unaiona hapo, ni wangapi waliona picha hizo? Vema ni hakika nimeona. Vema, hivyo ndivyo Kristo alivyo Mwenywe, injili ule ujumbe ulivyo. Utakapoona ujumbe mara moja tu wa saa, hakuna kitu kingine

chochote uonacho ila huo. Hivyo ndivyo ilivyo kitu kingine chochote kinaondoka. Vingine ni vya kujazia tuu, ukiishaona ule ujumbe mara hiyo ilikuwa hivyo wakati wa nuhu, wakati Nuhu na kundi lake walipoona ule ujumbe wao vitu vingine vyote havikuwa na maana. Wakati lile kundi la mitume walipoona hilo vitu vingine havikuwa na maana, wakati kundi la Luther walipoona hilo, kundi la Wesley walipoona hilo, kundi la pentekoste walipoona hilo, hakuna kitu kingine walichokijali walijitenga mbali na vitu vinginevyo kwa nini? Kwa ufahamu wake wa kimbele alikuwa amevichagua vitu hivi vitoke [2]

Yeye ni kiini kikuu cha Biblia yote kama unasoma Biblia na humuoni Kristo kwa kila mstari wake unapaswa urudi nyuma usome tena unaona? Kama huwezi kumuona Kristo katika kila mstari wa Biblia unapaswa usome tena kwa sababu kuna kitu fulani ambacho umekikosa. Biblia ni Kristo, Yeye ni Neno unaposoma ‘hapo mwanzo Mungu aliumba.....” huyo hapo Kristo, unaona? Kutoka hapo mpaka “Amina” katika ufunuo kila Neno linamshuhudia Yesu Kristo [1].

Angalia, Waisraeli wote kati ya makumi elfu ambao walikuwepo katika siku hizo (makisio ni milioni nne).....Na kulikuwa na mia moja na ishirini waliosikia sauti yake, hati ya milioni nne kama unyakwaji utakuja leo itakuwa inatisha kama nitawaambia vile ninavyofikiri itatokea hiyo ni kweli. Kuna wengi waitwao wakristo waliojaa dunia nzima , ni vitu vya kujazia bustani ionyeshayo sanamu fulani, ile sanamu ndio kitu cha kuangalia, Kristo ndiyo sura yenyewe hivyo ni kweli na lile kanisa la kweli la waliozaliwa mara ya pili ndilo hilo ambalo Yeye anakuja kuchukuwa waliobaki ni vitu vya kujazia tuu hiyo ni kweli [3].

Ile siri kuu ya Mungu siku zote imewapofusha wenye hekima wa dunia (1kor.2:6-10). Hawakuweza kuielewa hiyo, shetani haielewi hiyo na hakuna hata anayejiielewa miongoni mwa wengine ila tuu wale ambao wamekusudiwa kimbele kuielewa hiyo. Vile Mungu na Kristo walivyo mmoja watamfanya kuwa (nafsi tatu) watatu kila mara unaona? Hakika wao hufanya hivyo. Angalia kifuatacho.....cha pili, udhihirisho wa Kristo ndani yako, tumaini la utukufu, yule Mungu mkuu aliye dhihirishwa ndani ya Kristo sasa Kristo alidhihirishwa ndani yako.

Tazama, ile iliyokuwa siri kuu ya Mungu mwanzoni, siri kuu ilifichwa katika nia yake inawekwa sasa katika mioyo ya waaminio ambao ni mwili wa Kristo. Ile iliyokuwa ni siri kuu ya Mungu mwanzoni iliyokuwa katika nia yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu sasa umedhihirishwa fikiria hilo marafiki. Oh ninauhakika hatulielewi hilo vema silioni kama mnavyopaswa kuliona, na ninauhakika hamliani. Unaona? Lakini ile siri kuu ya Mungu, ambayo Mungu wa milele alikuwa nayo, hana siri, sasa imewekwa wazi ndani ya Yesu Kristo, halafu sasa Yeye analipa kanisa lake huku chini kile kilichikuwepo katika nia/mawzo ya Mungu. Sasa kimo ndani ya mwili wa Kristo, Yesu alifanya mapenzi na kanisa, bibi harusi wake, akilinong’oneza siri zake. Unajua unayomwambia mke wako mambo unajua yule msichana mdogo unaye enda kumuoa unampenda sana sana, unamwambia yeye mambo ya siri na kumuambia nia ili moyo wake ukuelekee wewe na akupende wewe na vinginevyo,

unajua vile ulivyo? Hivyo ndivyo Kristo anavyofanya kwa kanisa, unaona? Anamuacha yeye ajue zile siri. Siyo kama viruka njia na maanisha mke wake, unaona Anamuacha yeye ajue zile siri, zile siri tu. Siyo hawa viruka njia na anamaanisha mke wake unaona? Vema

Angalia hilo akiwa ana ule ufunuo wa ile siri yake, akiwajulisha hao kwa neema .Angalia wakati huu ufunuo mkuu, uliifunua ile siri ijulikane kwako, hapo sasa unadharau vitu vyote vya dunia [1].

Nukuu za kiingereza:

1: Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa (63-0728), uk 16-17, 19-21,25,27,36,57-59.

2: Kujaribu kumtendea Mungu kazi (65-1127B)-aya 135-138.

3: Sauti zisizo za uhakika (62-0714)aya 62.

Jiwe la kujengea la kiroho nambari 200 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendstr. 69.D-75328 Schomberge Germany Simu (+49) 2357613 Fax 72353306.

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia.

Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk724.)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@livel.com

Cellphone: 0784 704299/ 0713230098